مسواک شریف کے فضائل (Swahili)

# Fadhila za Miswak




Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**

**Attar Qadiri Razavi**

مِسواک شَرِیف کے فَضائل

Miswak Shareef kay Fazaail

# Fadhila za Miswak

**KITABU HIKI** KILITOLEWA KWA KIURDU NA MAJLIS AL-MADINAH-TUL-'ILMIYYAH. IDARA YA TAFSIRI (DAWAT-E-ISLAMI) IMETAFSIRIWA kwa Kiswahili. Ukipata kosa lolote katika tafsiri au utunzi, tafadhali ijulishe Idara ya Tafsiri kwenye anwani ifuatayo ya posta au barua pepe kwa nia ya kupata malipo [Sawab].

**Idara ya tafsiri (Dawat-e-Islami)**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

**UAN:** ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 7213

**Barua pepe:** translation@dawateislami.nets

**Fadhila za Miswak**

Tafsiri ya Kiswahili ya 'Miswak Shareef kay Faza`il'

◆

## HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA

Hakimiliki © 2024 Maktaba-tul-Madinah

Hairuhusiwi kunakili, au kusambaza sehemu yoyote ya chapisho hili kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodiwa au vinginevyo, bila ya idhini ya maandishi ya Maktaba-tul-Madinah.

| | |
|---|---|
| **Chapisho la kwanza:** | Shawwal-ul-Mukaram, 1445 AH (April, 2024) |
| **Imetafsiriwa na:** | Translation Department (Dawat-e-Islami) |
| **Mchapishaji:** | Maktaba-tul-Madinah |
| **Kiasi:** | 3000 |

### UFADHILI

Tafadhali jisikie huru kuwasiliana nasi ikiwa ungependa kufadhili uchapishaji wa kitabu cha kidini au kijitabu kwa ajili ya Isal-e-Sawab ya wanafamilia wako waliofariki.

**Maktaba-tul-Madinah**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah Mahallah Saudagran,
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

**Barua pepe:** maktabaglobal@dawateislami.net –
maktaba@dawateislami.net

**Simu:** +92-21-34921389-93

**Tovuti:** www.dawateislami.net



www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى خَاتَمِ النَّبِيّٖن،
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# Dua ya kusoma kitabu

Soma Du'a ifuatayo (dua) kabla ya kusoma kitabu cha dini au somo la Kiislamu, utakumbuka chochote ulichokisoma, اِنْ شَآءَ اللّٰه:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

## Tafsiri

**Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Tufungulie milango ya elimu na hekima, na utuhurumie! Ewe Ambaye ni Mtukufu na Mwenye heshima!**

*(Al-Mustatraf, Juzuu ya 1, Uk. 40)*

**Kumbuka:**

Mswalie Mtume ﷺ mara moja kabla na baada ya Du'a.



www.dawateislami.net

# Jedwali la Yaliyomo


Fadhila za Miswak ..... 1
Ubora wa Swala - 'Alan -Nabiy ﷺ ..... 1
Ni wakati gani mtu hapati thawabu ya kutumia Miswak? ..... 1
Misemo10 yaliyobarikiwa ya Rasuul mpenzi ﷺ kuhusu Miswak ..... 2
Kupiga Miswaki huimarisha kumbukumbu ..... 3
Fursa ya kusoma Kalimah wakati wa kifo ..... 4
Vitendo vya kuongeza akili (ufahamu) ..... 4
Rasuul mtukufu ﷺ alikuwa akipiga Miswaki wakati gani? ..... 4
Miswaki kwa kila Swalah ..... 4
Kutumia Miswak wakati wa kuamka ni Sunnah ..... 5
Hatua ya kwanza wakati wa kuingia nyumbani ..... 5
Miswak katika hali ya Sawm [kufunga] ..... 6
Baadhi ya lulu za Madani kuhusu Miswak wakati wa kufunga Swaum ..... 6
Miswak kabla ya kuondoka kwa dhahiri ..... 6
Ni Sunnah kwa msafiri kuweka vitu 8 kwake ..... 7
Miswak kabla ya kula ..... 7
Ushauri wa kuondoa unjano kwenye meno ..... 8
Sababu ya asilimia themanini (80%) ya magonjwa ..... 8
Faida za kiafya za Miswak ..... 8
Miswak hutibu asidi ya tumbo na vidonda mdomoni! ..... 9
Du'a kwa ajili ya Miswak ..... 10
Lulu 14 za Madani za Miswak ..... 11
Mbinu ya kutumia Miswak ..... 12
Kwa wanawake, ni Sunnah ya Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah kufanya Miswak. ..... 12
Wakati Miswak inakuwa isiyoweza kutumika ..... 13
Je! unajua jinsi ya kufanya Miswak? ..... 13

Mifumbo na masimulizi kumi za wapenzi wa Miswak.............................14
1. Miswak Iliyopinda..........................................................................14
2. Kunyonya Miswak ni vipi?...................................................................14
3. Miswak katika ʻImamah (Kilemba) ......................................................15
4. Miswak kwenye sikio ..........................................................................15
5. Miswak iliyofungwa kwa kamba shingoni..............................................15
Mtu anapaswa kuacha Mustahab ikiwa kuna khofu ya Fitnah.................16
Kuweka kalamu kwenye sikio..................................................................17
Tengeneza mfuko maalum wa kuweka Miswak .......................................17
6. Miswak ilinunuliwa kwa sarafu ya dhahabu (kisa)................................18
7. Machozi yalitoka machoni! (Kisa) ........................................................19
8. Miswak iliponya kuvimba kwa shingo na koo .......................................20
9. Miswak na tezi za koo *(throat glands)*.................................................21
10. Baraka 25 za Miswak...........................................................................21
Madani Qafilah ........................................................................................23
Bibliografia ...............................................................................................24



www.dawateislami.net

اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ رَبِّ الۡعٰلَمِیۡنَ وَ الصَّلٰوۃُ وَ السَّلَامُ عَلٰی خَاتَمِ النَّبِیّٖن،
اَمَّا بَعۡدُ فَاَعُوۡذُ بِاللّٰہِ مِنَ الشَّیۡطٰنِ الرَّجِیۡمِ ؕ بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ ؕ

# Fadhila za Miswak

Haijalishi Shetani anajaribu sana kukufanya ujisikie mvivu, tafadhali soma kitabu hiki kuanzia mwanzo mpaka mwisho, اِنۡ شَآءَاللّٰہعَزَّوَجَلَّ utakuza mapenzi makubwa kwa ajili ya Miswak.

## Ubora wa Swala - 'Alan -Nabiy ﷺ

Rasuli Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kunisomea Swala mara 50 katikia siku moja nitapeana mkono naye Siku ya Hukumu.' *(Ibn Bishkwal, pp. 90, Hadees 90)*

صَلُّوۡا عَلَی الۡحَبِیۡب صَلَّی اللّٰہُ عَلٰی مُحَمَّد

## Ni wakati gani mtu hapati thawabu ya kutumia Miswak?

Matendo yanatokana na nia, ikiwa hakuna nia njema, basi hakuna malipo mema yanayopatikana. Kwa hiyo, kabla ya kutumia Miswak, fanya nia ifuatayo: *Ili kupata malipo ya Sunnah, nitatumia Miswak na kupitia njia hiyo, nitasafisha kinywa changu kwa ajili ya kusoma Qur'ani Tukufu, Zikr ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na Salat -'Alan -Nabi.*

## Misemo10 yaliyobarikiwa ya Rasuul mpenzi ﷺ kuhusu Miswak

1. Kuswali rakaa 2 baada ya kufanya Miswak ni bora kuliko rakaa 70 bila ya Miswak.

   *(Attargheeb Wattarheeb, juzuu ya 1, uk. 102, Hadees 18)*

2. Kuswali Swalah baada ya kufanya Miswak ni bora mara 70 kuliko Swalah iliyoswaliwa bila [kutumia] Miswak. *(Shu'ab-ul -Iman, juzuu ya 3, uk. 26, Hadiyth 2774)*

3. Vitendo vinne vilivyobarikiwa ni Sunnah ya Rusul iliobarikiwa: (1) Kuvaa 'Itr (kupaka manukato) (2) Kufanya Nikah (Kufunga ndoa) (3) Kutumia Miswak (4) Kuwa na staha.

   *(Musnad Imam Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 9, uk. 147, Hadiyth 23641)*

4. Tumia Miswaki! Usinikaribie na meno ya njano. *(Jam'- ul -Jawami', juzuu ya 1, uk. 389, Hadiyth 2875)*

5. Kuna tiba ya kila ugonjwa katika Miswak isipokuwa kifo. *(Jami' Sagheer, uk. 297, Hadees 4840)*

6. Lau nisingehisi kuwa itakuwa vigumu juu ya Ummah wangu, ningewaamrisha kutumia Miswak katika kila Wudhu. *(Sahih Bukhari, juzuu ya 1, uk. 637)*

7. Yafanye matumizi ya Miswak kuwa ya lazima kwako mwenyewe kwa sababu ndani yake kuna usafi wa kinywa

na ni njia ya kupata radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ. *(Musnad Imam Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 2, uk. 438, Hadiyth 5869)*

8. Wudhu ni nusu ya Iman, na kutumia Miswak ni nusu ya Wudhu. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juzuu ya 1, uk. 197, Hadiyth 22)*

9. Wakati mtu anaposimama kwa ajili ya Swalah baada ya kufanya Miswak, Malaika husimama nyuma yake akisikiliza kisomo chake, kisha humkaribia hadi pale Malaika anaweka mdomo wake juu ya mdomo wa msomaji.
*(Al-Bahr-uz-Zakhaar, juzuu ya 2, uk. 214, Hadiyth 603)*

10. Yeyote anayeoga siku ya Ijumaa, akafanya Miswak, akapaka 'Itr (manukato), avae nguo nzuri kisha akaja Msikitini na hakanyagi watu, lakini huswali na hunyamaza kimya baada ya kuwasili kwa Imam (yaani wakati wa Khutbah) mpaka kukamilika kwa Swalah, Allah عَزَّوَجَلَّ humsamehe madhambi yake yote aliyoyatenda katika wiki hiyo.
*(Musnad Imam Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 4, uk. 162, Hadiyth 11768)*

## Kupiga Miswaki huimarisha kumbukumbu

Ameer-ul-Mu`mineen Sayyiduna Ali كَرَّمَ اللّٰهُ وَجْهَهُ الْكَرِيْم amesema, ‘Mambo matatu yanaimarisha kumbukumbu na huondosha balaghamu (1) Mswaki (2) kufunga saumu (3) Kusoma Quran tukufu.' *(Ihya- ul- 'Uloom, juzuu ya 1, uk. 364)*

## Fursa ya kusoma Kalimah wakati wa kifo

Katika Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, ukurasa wa 288, iliyochapishwa na Maktaba- tul -Madinah; idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami, imeeleza: Yeyote mwenye mazoea ya [kutumia] Miswaki atabahatika kusoma Kalimah wakati wa kifo na yeyote atakayetumia kasumba hatabahatika kusoma Kalimah wakati wa kifo.

## Vitendo vya kuongeza akili (ufahamu)

Sayyiduna Imamu Shaafi'i رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mambo manne yanaongeza akili: (1) Kujiepusha na mazungumzo ya upuuzi (2) Kutumia Miswaki (3) Kujihusisha na Kundi la watu wachamungu (4) Kutenda juu ya elimu aliyobarikiwa nayo mtu.

*(Hayat-ul-Haywan lid- Dameeri, juzuu ya 2, uk. 166)*

## Rasuul mtukufu ﷺ alikuwa akipiga Miswaki wakati gani?

### Miswaki kwa kila Swalah

Sayyiduna Zayd Bin Khalid Juhani رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ amesema, Rasuli kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hataiacha nyumba yake iliyobarikiwa kwa ajili ya Swalah yoyote mpaka yeye صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم awe ametekeleza utumiaji wa Miswak. *(Al Muujam-ul-Kabeer lit-Tabarani, juzuu ya 5, uk. 254, Hadithi 5261)*

## Kutumia Miswak wakati wa kuamka ni Sunnah

Imepokewa kutoka kwa Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِیَ اللہُ عَنْہَا: Miswak na maji ya wudhu yalikuwa yakiwekwa kwa ajili ya Rasuli kipenzi صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم Wakati Yeye صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akiamka usiku, kisha baada ya kutimiza haja, Yeye صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alikuwa kwanza akitumia Miswaki. *(Abu Dawood, juz. 2, Hadithi 56)*

Katika Hadiyth nyingine iliyobarikiwa, vile vile imepokewa kutoka kwa Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِیَ اللہُ عَنْہَا: Wakati wowote Rasuli Kipenzi صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم angeamka kutoka usingizini; mchana au usiku, Yeye صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alikuwa akifanya Miswak kabla ya Wudhu.

*(Ibid, Hadiy 57)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kufanya Miswak baada ya kuamka ni Sunnah. Wakati wa kulala, gesi za tumbo zenye harufu mbaya husafiri hadi mdomoni,na kwa sababu yake harufu mbaya na mabadiliko ya ladha hutokea kinywani. Kupitia baraka ya Sunnah hii, mdomo unakuwa safi.

## Hatua ya kwanza wakati wa kuingia nyumbani

Sayyiduna shurayh Bin Haani رَحْمَۃُ اللّٰہِ عَلَیۡہ anasimulia kwamba nilimuuliza Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِیَ اللہُ عَنْہَا Wakati Mtume mtukufu صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم aliingia nyumbani, Yeye صَلَّی اللہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alikuwa akifanya nini mwanzo kabisa?' Yeye رَضِیَ اللہُ عَنْہَا akajibu, 'Miswak.' *(Sahih Muslim, uk. 152, Hadiyth 253)*

## Miswak katika hali ya Sawm [kufunga]

Imepokewa kutoka kwa Sayyiduna ‘Aamir Bin Rabiy’ah رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُمَا: Nilimuona Rasuli Kipenzi صَلَّی اللّٰہُ عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akitumia Miswak mara nyingi wakati wa kutekeleza Sawm (صَوْم).

*(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 2, uk. 176, Hadees 725)*

## Baadhi ya lulu za Madani kuhusu Miswak wakati wa kufunga Swaum

Imeelezwa katika Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, ukurasa wa 997: Sio Makruh [karaha] kufanya Miswak wakati wa kufunga Swaum, bali kwa hakika kama ilivyo Sunnah katika siku nyingine, pia ni Sunnah wakati wa kufunga Swaum. Iwapo Miswak ni mkavu au yenye unyevunyevu, ikiwa na unyevu unyevu sababu ya maji, iwe inatumika kabla ya Zawaal au baada yake; sio Makruh (karaha) wakati wowote. Imezoeleka miongoni mwa watu wengi kuwa ni Makruh (karaha) kufanya Miswak mchana; hii ni kinyume na Madhhab ya Hanafi. *(Bahar- e -Shari’at, juzuu ya 1, uk. 99)*

Iwapo kwa kutafuna Miswak, athari [za nyuzi za Miswak] zimeachwa au ladha inahisiwa mdomoni, basi mtu hatakiwi kufanya Miswak kwa namna hiyo akiwa amefunga Swaum. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 10, uk. 511)*

## Miswak kabla ya kuondoka kwa dhahiri

Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہَا alisema kwamba wakati wa

kuondoka kwa dhahiri, nilimuomba Rasuli kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم 'Je, nilete Miswak?' Rasuli kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akaitikia kwa kukubali kwa ishara ya kichwa. Basi mimi baada ya kuipokea kutoka kwa (ndugu yangu) Sayyiduna 'Abdur Rahman رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ, nikamkabidhi kipenzi Rasuli صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Yeye صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alitaka kuitumia lakini ulikuwa mgumu sana, kwa hiyo, nikaomba, 'Je, niulainishe?' Rasuli Kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alitikisa kichwa chake kilichobarikiwa kukubali. Hivyo, baada ya kulainisha Miswak kwa kuitafuna kwa meno yangu, niliiwasilisha kwake. Yeye صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kisha akaanza kuisogeza juu ya meno yake yaliyobarikiwa.

*(Imefupishwa kutoka: Sahih Bukhari, juzuu ya 1, 3, uk. 308, 157, 890, Hadees 4449)*

## Ni Sunnah kwa msafiri kuweka vitu 8 kwake

Baba mtukufu wa Imamu wa Ahl-us-Sunnah, Imam Ahmad Raza Khan, Maulana Naqi 'Ali Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Rasuli kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akiweka kwake vitu 8 anapokuwa safarini. (1) Miswak (2) Kohl (wanja) (3) Kioo (4) Kichana (5) Mkasi (6) Sindano (7) Uzi. (Anwaar Jamal- e - Mustafa, uk. 160) Katika riwaya nyingine, (8) 'Mafuta' (pia) yametajwa. *(Subul- ul -Huda, juzuu ya 7, uk. 347)*

## Miswak kabla ya kula

Sayyiduna 'Abdullah Bin 'Umar رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُمَا alikuwa akifanya Miswak kabla ya kula. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juzuu ya 1, uk. 197)*

## Ushauri wa kuondoa unjano kwenye meno

Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ anasema: Kufanya Miswak baada ya kula huondoa madoa ya manjano kutoka kwenye meno. *(Al-Kamil fi Du'afa-ir-Rijaal, juzuu ya 4, uk. 123)*

## Sababu ya asilimia themanini (80%) ya magonjwa

Kulingana na utafiti wa wataalamu, 80% ya magonjwa husababishwa na matatizo ya meno na tumbo. Kwa ujumla, kutokana na kutotunza meno, aina kadhaa za bakteria hukusanyika kwenye ufizi na kisha kwenda kwenye tumbo, na kusababisha magonjwa mengi.

## Faida za kiafya za Miswak

- Kulingana na utafiti wa kampuni maarufu ya Marekani, Miswak ina uwezo wa asilimia ishirini (20%) zaidi kuliko njia nyingine yoyote katika kuondoa bakteria hatari.
- Kulingana na uchunguzi mmoja wa wanasayansi fulani wa Uswidi, rasha za Miswak huondoa bakteria moja kwa moja bila kuzitafuna na kulinda meno kutokana na magonjwa mengi.
- Imetajwa katika utafiti uliochapishwa wa Maktaba ya Kitaifa ya Dawa ya Marekani kwamba ikiwa Miswak itatumiwa kwa usahihi, ni njia bora ya kusafisha meno na kinywa; pia, ya kuimarisha ufizi.

- Kulingana na utafiti mmoja, wale watu wanaotumia Miswak mara kwa mara, wana malalamiko machache kuhusu kutokwa na damu kwenye ufizi.
- Ilitajwa katika mkutano uliofanyika Atlanta, Amerika kuhusiana na meno, kwamba kuna vitu kama hivyo katika Miswak vinavyolinda meno kutokana na udhaifu, na Miswak ina manufaa zaidi kuliko aina zote za dawa zinazotumiwa kusafisha meno.
- Miswak huondoa tabaka za utando kwenye meno.
- Miswak hulinda meno yasivunjike au kukatika.
- Wakati wagonjwa wa baridi na mafua ya kuendelea ambao hawawezi kuondoa balaghamu, hutumia Miswak, balaghamu huondolewa; na hivyo wanaanza kuhisi wepesi kichwani.
- Imethibitishwa kutokana na uzoefu na utafiti wa wanapatholojia kwamba Miswak ni tiba bora ya baridi inayoendelea.

## Miswak hutibu asidi ya tumbo na vidonda mdomoni!

Vidonda vingine huonekana kinywani kwa sababu ya asidi ya tumbo. Kuna aina moja kama hiyo kwa sababu ambayo bakteria nyingi huenea; kwa hivyo mtu atumie Miswak mbichi pamoja na mate yanayotokana nayo. اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ ugonjwa

huo utaondoka. Watu wengine wanalalamika kwamba meno yao yanageuka manjano au utando mweupe hutoka. Miswak iliyo na *rasha* mpya ni ya manufaa kwa watu kama hao, na pia ni ya manufaa kwa kuondoa unjano kutoka kwa meno. Miswak huondoa harufu mbaya na bakteria kutoka kinywani, na humwokoa mtu kutokamana na magonjwa kadhaa.

## Du'a kwa ajili ya Miswak

Baadhi ya mafaqihi watukufu رَحِمَهُمُ اللّٰه wanasema; Soma Du'a ifuatayo wakati wa kutumia Miswak:

﴾1﴿ اَللّٰهُمَّ بَيِّضْ بِهٖ اَسْنَانِيْ، وَ شُدَّ بِهٖ لِثَاتِيْ، وَ ثَبِّتْ بِهٖ لَهَاتِيْ، وَ بَارِكْ لِيْ فِيْهِ، يَا اَرْحَمَ الرّٰحِمِيْن[1]

---

[1] ***Tafsiri*:** Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Kupitia hiyo, yafanye meupe meno yangu, itie uimara ufizi wangu na koo langu, na nipe baraka ndani yake, Ewe Mwingi wa rehema kuliko wenye kurehemu! *(Sharh-ul-Muhazzab lin-Nawavi, juzuu ya 1, uk. 283)*

﴾2﴿ اَللّٰهُمَّ طَهِّرْ فَمِىْ، وَ نَوِّرْ قَلْبِىْ، وَ طَهِّرْ بَدَنِىْ، وَ حَرِّمْ جَسَدِىْ
عَلَى النَّارِ، وَ اَدْخِلْنِىْ بِرَحْمَتِكَ فِىْ عِبَادِكَ الصّٰلِحِيْن[1]

**Lulu ya Madani:** Mtu anaweza kusoma Du’a zote mbili au mojawapo.

## Lulu 14 za Madani za Miswak

1. Miswak inapaswa kuwa ya Peelu au mbao chungu kama vile mzeituni nk.
2. Unene wa Miswak unapaswa kuwa sawa na ule wa kidole kidogo.
3. Haipaswi kuwa ndefu zaidi ya urefu wa mkono, vinginevyo Shetani huketi juu yake.
4. Ni sharti rasha ziwe laini kwa sababu rasha ngumu husababisha mapengo kati ya meno na ufizi.
5. Miswak kuwa mbichi ni bora vinginevyo ifanye iwe laini kwa kuiweka kwenye glasi ya maji kwa muda.
6. Madaktari wanashauri kukata rasha za Miswak kila siku.

---

[1] ***Tafsiri*:** Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Safisha kinywa changu, utie nuru moyo wangu, utakase mwili wangu, na ufanye moto wa Jahannam kuwa ni Haramu kwenye mwili wangu na kutokana na Rehema Yako, nijumuishe miongoni mwa watu wema! *(‘Umda-tul-Qaari, juzuu ya 5, uk. 31, Hadiyth 887)*

## Mbinu ya kutumia Miswak

7. Piga Miswaki kwa njia ya mlalo kwenye meno.

8. Wakati wowote mtu anapopiga Miswaki, inapaswa kufanywa hivyo angalau mara tatu kwa kuosha kila wakati.

9. Shika Miswak katika mkono wa kulia kwa namna ambayo kidole kidogo kibaki chini yake, na vidole vitatu vya kati vibaki juu yake huku kidole gumba kikibaki kwenye ncha ya juu ya rasha ya Miswak. Kwanza safisha safu ya juu ya kulia ya meno na kisha safu ya juu kushoto. Kisha safisha safu ya chini ya kulia na kisha safu ya chini ya kushoto ya meno.

10. Kupiga Mswaki huku ukiishika kwa namna ya ngumi kunaweza kusababisha milundo.

11. Miswak ni Sunnat-e-Qabliyyah [kwa maneno mengine, Miswak ni Sunnah ya kabla ya Wudhu, si wakati wa Wudhu] kwa hiyo tumia Miswak kabla ya kuanza Wudhu, kisha osha mikono yote miwili mara tatu na (Wudu kamili) kama kawaida. Hata hivyo, inakuwa ni Sunnah Muakkadah kunapokuwa na pumzi mbaya. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 1, uk. 837)*

## Kwa wanawake, ni Sunnah ya Sayyidatuna ‘Aaishah Siddiqah kufanya Miswak.

12. Imesemwa katika Malfuzaat A'la Hadrat kwamba: Kwa



www.dawateislami.net

wanawake ni Sunnah ya Umm-ul-Mu`mineen Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهَا kutumia Miswak lakini wasipotumia Miswak basi hakuna ubaya katika jambo hilo. Meno na ufizi zao ni khafifu kwa kulinganisha na wanaume; itatosha wakitumia Missi (gome la mti kusafisha meno). *(Malfuzaat A'la Hadrat, uk. 357)*

## Wakati Miswak inakuwa isiyoweza kutumika

13. Wakati Miswak inapokuwa haitumiki, mtu hatakiwi kuitupilia mbali kwani hiki ni chombo cha kufanyia kazi Sunnah. Inapaswa kuwekwa mahali fulani kwa uangalifu; au kuzikwa mahali fulani au kufungwa kwenye jiwe na kuzamishwa baharini. *(Kwa maelezo ya kina, tafadhali rejelea Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, ukurasa wa 294-295; kilichochapishwa na Maktaba- tul -Madinah.)*

## Je! unajua jinsi ya kufanya Miswak?

14. Inawezekana kwamba ingawa unahisi kuwa umekuwa ukitumia Miswak kwa muda mrefu, hata hivyo una matatizo ya meno na tumbo! Ndugu zangu wapenzi wa Kiislamu! Si kosa la Miswak bali ni lako mwenyewe. Mimi (Sag- e -Madinah) nimefikia hitimisho kwamba siku hizi, pengine mmoja kutoka kwa maelfu anajua jinsi ya kutumia Miswak kwa usahihi. Kwa kawaida tunaharakisha baada ya kusugua Miswak kwenye meno yetu katika Wudhu (udhu), kwa maneno mengine, inapaswa kusemwa

kwamba kwa hakika hatufanyi Miswak ipasavyo; kwa kweli ni urasmi wa Miswak badala ya kufanywa kwa haraka.

◆◆◆

## Mifumbo na masimulizi kumi za wapenzi wa Miswak

### 1. Miswak Iliyopinda

Mahali fulani, Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipata Miswak miwili, mmoja ukiwa umepinda na mwingine ulio nyooka. Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akampa mwenzake ulio nyooka, na akajiwekea uliopinda. Swahaba akasema kwa unyenyekevu: Ya Rasuolallah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Unastahiki zaidi Miswak ambayo ni sawa! Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akajibu: Kila mtu anapofanya usuhuba wa mtu, hata ikiwa ni kwa ajili ya muda mfupi wa siku moja, ataulizwa masuali kuhusu hilo siku ya kiyama. *(Imefupishwa kutoka: Qoot- ul -Quloob, juzuu ya 2, uk. 387; Ihya- ul -'Uloom, juzuu ya 2, uk. 218)*

### 2. Kunyonya Miswak ni vipi?

Kuhusu kipande cha habari kilichotajwa katika kitabu Durr- e -Mukhtar, yaani, kunyonya Miswak kunasababisha upofu, imeelezwa katika Fatawa Shaami: Kuhusu kitendo cha kumeza mate bila kunyonya Miswak, Hakeem Tirmizi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema; Wakati wa kutumia Miswak, mtu anapaswa kumeza

mate ambayo hutolewa mwanzoni kwa sababu huponya magonjwa yote isipokuwa *leukoderma*, ukoma na kifo.

*(Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 1, uk. 251)*

## 3. Miswak katika 'Imamah (Kilemba)

Imeelezwa katika Fatawa Shaami kwamba baadhi ya masahaba waliobarikiwa رَضِیَ اللّٰہ عَنْهُم wangeweka Miswak yao kati ya mikunjo ya 'Imamah (Kilemba) zao.

## 4. Miswak kwenye sikio

Sayyiduna Zayd Bin Khalid Juhani رَضِیَ اللّٰہ عَنْهُ angeenda Msikitini kuswali Swalah akiwa ameweka Miswak kwenye sikio lake, kama kalamu inavyowekwa kwenye sikio la mwandishi.

## 5. Miswak iliyofungwa kwa kamba shingoni

Imeelezwa katika ukurasa wa 402 wa kitabu chenye kurasa 518, 'Imamay kay Fazaail' [Ubora wa 'Imamah] kilichochapishwa na Maktaba- tul -Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat- e - Islami: Sayyiduna Imam 'Abdul Wahhab Sha'rani رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Tumewekewa ahadi kuwa tutatumia Miswak mara kwa mara kabla ya kila wudhuu na Swalah, hata kama wengi wetu watalazimika kufunga Miswak yetu kwa kamba shingoni mwetu (ili Miswak isipotee) au hata ikibidi kuifungamanisha na kilemba chetu pale 'Imamah inapofungwa bandani tu. Ikiwa tutakuwa na kofia, tutaifunga 'Imamah juu yake kwa nguvu na



www.dawateislami.net

tutaiambatanisha Miswak kwenye Imamah kuelekea sikio la kushoto. *(Lawaqi- ul -Anwaar, juzuu ya 1, uk. 16)*

## Mtu anapaswa kuacha Mustahab ikiwa kuna khofu ya Fitnah

Mapenzi ya kina yaliyoje ya maswahaba waliobarikiwa رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُم na watangulizi wema رَحِمَہُمُ اللّٰہُ waliyokuwa nayo kwa ajili ya Miswak! Na mamilioni ya sifa ziwe juu ya matendo yao matukufu! Kumbuka! Siku hizi, kama mtu akitangatanga mitaani akiwa ameweka Miswak sikioni mwake au kwenye 'Imamah (kilemba) au Miswak ikiwa imefungwa kamba shingoni, watu watamnyooshea kidole na kumdhihaki mtu kama huyo. Kwa hivyo, inapaswa kuepukwa mbele ya umma.

Kuhusu kitendo fulani cha Mustahab, A'la Hadrat رَحۡمَةُ اللّٰہِ عَلَیۡه aliulizwa swali. Kwa vile kulikuwa na hatari ya Fitnah endapo wataifanyia kazi kitendo hicho cha Mustahab huko India, A'la Hadrat رَحۡمَةُ اللّٰہِ عَلَیۡه akajibu: Popote palipozoeleka, ni Mustahab mahali hapo. Ama miji ya Kihindi ambako ni jambo lisilo la kawaida kabisa, na kama mtu yeyote akiifanyia kazi, basi watu wajinga wataifanyia mzaha, na kuifanyia mzaha hukumu ya Kiislamu kunaweza kuharibu Dini ya mtu - kwa hivyo hakuna haja ya kuchukua hatua juu yake (kuitenda) katika sehemu kama hizo. Iwapo Waislamu wanajiingiza katika suala zito (yaani kuzifanyia mzaha hukumu za Kiislamu), basi kutenda



www.dawateislami.net

kwa kitendo cha Mustahab haipendekezwi. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 603)*

## Kuweka kalamu kwenye sikio

Kwa mwandishi kuweka kalamu kwenye sikio lake ni jambo jema. Sayyiduna Zayd Ibn Saabit رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ amesema: Wakati fulani nilikuwepo kwenye baraza la Mtukufu Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Mbele yake kulikuwa na mwandishi. Nimemsikia Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akisema: Weka kalamu kwenye sikio lako, kwani humfanya mtu akumbuke sana anachokwenda kuandika. *(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 4, uk. 327, Hadees 2723)*

Mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه amesema kuhusu Hadiyth hii iliyobarikiwa: Ikiwa mwandishi ataweka kalamu sikioni mwake, atakumbuka mawazo anayokwenda kuyaandika. Ni bora kuweka kalamu kwenye sikio la kulia. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Ameumba athari fulani katika kila kitu. Athari ya kuweka kalamu kwenye sikio ni kwamba mtu anakumbuka mada. *(Mirat- ul -Manajih, juz. 6, uk. 334)* Hii inaweza pia kumaanisha athari ya kisaikolojia.

صَلُّوۡا عَلَی الۡحَبِيۡب صَلَّی اللّٰهُ عَلٰی مُحَمَّد

## Tengeneza mfuko maalum wa kuweka Miswak

Ikiwezekana, shona mifuko miwili kwa Kurta (kamisi) yako

[i.e. aina ya shati ndefu, iliyolegea na yenye mikono mirefu]; mmoja kulia na mwingine kushoto. Pia uwe na mfuko mdogo ulioshonwa ubavuni karibu na moyo (yaani upande wa mkono wa kushoto). Itakuwa kana kwamba Miswak - Sunna ya kipenzi chetu, Rasuli Mtukufu - صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم itashikamana na kifua na moyo.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## 6. Miswak ilinunuliwa kwa sarafu ya dhahabu (kisa)

Sayyiduna 'Abdul Wahhab Sha'rani رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesimulia: Mara moja, Sayyiduna Abu Bakr Shibli Baghdadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alihitaji Miswak alipokuwa akifanya wudhu. Aliutafuta lakini hakuupata. Basi yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akanunua Miswak kwa dinari moja (yaani sarafu ya dhahabu) na akaitumia. Baadhi ya watu wakamwambia, 'Umetumia pesa nyingi sana kwa ajili ya jambo hilo! Je, mtu atumie pesa nyingi kiasi hiki kwa Miswak?' Akajibu رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه 'Bila shaka, dunia hii na vyote vilivyomo havina thamani hata sawa na bawa la mbu katika mahakama ya Mwenyezi Mungu. Nitajibu vipi ikiwa, Siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ataniuliza, 'Kwa nini umeiacha Sunnah (Miswak) ya Kipenzi Changu Rasuli صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم? Uhalisia wa pesa na mali nilizokupa hazilingani hata kidogo na bawa la mbu katika mahakama yangu, basi baada ya yote, kwa nini hukutumia mali hiyo isiyo muhimu kwa ajili ya kukamilisha

Sunnah hiyo kubwa (Miswak)?′ *(Imefupishwa kutoka: Lawaqa-ul-Anwaar, uk. 38)*

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe bila ya hesabu kwa ajili yao!

اٰمِين بِجَاهِ خَاتَمِ النَّبِيّن صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

Enyi waja wa Rasuli! Mmeona? Upendo wa dhati ulioje wa watangulizi wetu wachamungu kwa ajili ya Sunnah iliyobarikiwa! Sayyiduna Abu Bakr Shibli رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alitumia dinari moja (yaani sarafu ya dhahabu) kwa ajili ya Miswak ambayo ni Sunna ya Mtukufu Nabii صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

## 7. Machozi yalitoka machoni! (Kisa)

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kila Sunnah ni hazina ya hekima. Chukua Miswak kama mfano! Vipi maneno yanaweza kueleza kikamilifu baraka za Sunnah hii! Mfanyabiashara mmoja alisema: Nilikutana na Muislamu mpya nchini Uswizi na nikampa zawadi ya Miswak. Aliipokea kwa furaha kubwa. Akaibusu Miswak kisha akaigusa machoni mwake. Mara machozi yakaanza kumtoka. Kisha akatoa leso mfukoni na kuifungua. Juu yake kulikuwa na Miswak ndogo takriban inchi mbili kwa urefu. Alisema aliposilimu, alipewa hiyo zawadi na Waislamu; aliitumia kwa uangalifu mkubwa na ilikuwa karibu kumalizika, na kumfanya awe na wasiwasi. Ilikuwa ni kwa neema ya Allah عَزَّوَجَلَّ kwamba alipokea zawadi nyingine ya



www.dawateislami.net

Miswak kutoka kwake, yaani kutoka kwa mfanyabiashara huyo.

Kisha akaongeza kuwa alikuwa na maambukizi ya muda mrefu katika meno na ufizi wake. Daktari wa meno hakuwa na tiba yake. Alianza kutumia Miswak na اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ baada ya siku chache, alijisikia vizuri. Alienda kumuona daktari ambaye alishangaa sana kuona amepona. Daktari alisema kuwa hawezi kuponywa kwa muda mfupi kwa kutumia dawa aliyoandikiwa. Kumbuka tu kile alichotumia. Alitafakari na kukumbuka kwamba alikuwa Muislamu na hivi karibuni alianza kutumia Miswak. Kwa sababu ya kutumia Miswak, alibarikiwa na kuponywa. Alipomuonyesha ile Miswak daktari, alishangaa.

## 8. Miswak iliponya kuvimba kwa shingo na koo

Mtu mmoja alikuwa na maumivu kwenye koo na shingo na pia alisumbuliwa na kuvimba kwa shingo. Sauti yake pia ilikuwa ya kishindo kutokana na ugonjwa wa koo. Alihisi kizunguzungu kutokana na maumivu na kuvimba kwa shingo yake. Kwa sababu hiyo, kumbukumbu yake pia ilikuwa dhaifu. Alipata matibabu lakini bila mafanikio. Siku moja, mtu fulani alimshauri kutumia Miswak; hivyo akaanza kuitumia mara kwa mara. Zaidi ya hayo, aliigawanya Miswak vipande viwili, akaiweka ndani ya maji, akaichemsha na kusukutukua kwa kutumia maji haya. Zaidi ya hayo, aliweka marhamu kwenye shingo mahali palipokuwa na uvimbe. Tiba hii imeonekana kuwa yenye ufanisi sana. Ilipochunguzwa, ilibainika kuwa tezi



www.dawateislami.net

zake *(thyroid glands)* pia ziliathiriwa, na kusababisha athari kwenye mwili wake wote. Ugonjwa huu uliondolewa kwa kutumia Miswak na akawa mzima.

## 9. Miswak na tezi za koo *(throat glands)*

Mtu alikuwa na wasiwasi juu ya tezi zake za koo zilizopanuliwa. Alichukua sharubati iliyotengenezwa kwa *mulberry* na pia akaanza kutumia Miswak safi mara kwa mara; yeye (mgonjwa) alianza kuhisi faida mara moja.

## 10. Baraka 25 za Miswak

'Allamah Sayyid Ahmad Tahtaawi Hanafi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameeleza manufaa na ubora wa Miswak katika kitabu Haashiyah Tahtaawi:

1. Fanya matumizi ya Miswak iliyobarikiwa kuwa muhimu kwako. Usighafilike nayo. Itumie mara kwa mara kwa sababu radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ zimo ndani yake.

2. Matumizi ya mara kwa mara ya Miswak hurahisisha kupata riziki na huleta baraka katika riziki.

3. Huondoa maumivu ya kichwa.

4. Huondoa kohozi.

5. Inaboresha macho.

6. Hudumisha utendakazi mzuri wa tumbo.
7. Humtia nguvu mtu anayeitumia.
8. Inaboresha kumbukumbu na kuongeza akili.
9. Husafisha moyo.
10. Matendo mema huongezeka.
11. Malaika huridhika.
12. Miswak inamchukiza Shetani.
13. Husaidia katika usagaji wa chakula.
14. Huongeza idadi ya kuzaliwa kwa watoto wa mtu.
15. Huchelewesha kuzeeka.
16. Huimarisha mgongo.
17. Huupa mwili nguvu kumtii Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ.
18. Huleta urahisi wakati wa kifo na humkumbusha mmoja kuhusu Kalimah wakati huo.
19. Ni njia ya kusababisha kupewa kwa kitabu cha matendo cha mtumiaji wa Miswak katika mkono wake wa kulia.
20. Inamfanya avuke Pul-Siraat kwa kasi ya umeme.
21. Mtu anayetumia Miswak husaidiwa katika kutimiza mahitaji yake.



www.dawateislami.net

22. Anapata amani na faraja kaburini.
23. Milango ya Peponi inafunguliwa kwa ajili yake.
24. Yeye ni msafi wakati wa kuondoka kutoka ulimwengu huu.
25. Faida kubwa kuliko yote ni kwamba radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ zimo ndani yake.

*(Imefupishwa kutoka: Haashiyah Tahtaawi, uk. 68-69)*

## Madani Qafilah

Safiri katika Madani Qafilah yenye msukumo wa Sunnah pamoja na waja wa Rasuul kwa ajili ya kujifunza Sunnah zilizobarikiwa, jaza kijitabu cha Madani In'amaat kwa kufanya Fikr-e-Madinah kila siku na ukikabidhi kwa ndugu wa Kiislamu anayehusika katika tarehe ya kwanza ya kila mwezi wa Madani. Kwa baraka zake, utajenga fikra ya kutenda juu ya Sunnah ya kutumia Miswak, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ.

Ewe Mola wa Mustafa! Kwa ajili ya Rasuli Wako Kipenzi صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, tujaalie upendeleo wa kuifanyia kazi Sunnah iliyobarikiwa ya kutumia Miswak.

اٰمِیْن بِجَاہِ خَاتَمِ النَّبِیّٖن صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

**Muhammad Ilyas Attar Qaadiri**
Rabi'- ul -Awwal 1438 AH (Desemba, 2016)

## Bibliografia

‘Umda-tul-Qaari, Dar-ul-Fikr, Beirut
Abu Dawood, Dar Ihya-ut-Turas Al-‘Arabi, Beirut
Al-Bahr-uz-Zakhaar, Maktaba-tul-‘Uloom wal-Hikm, Madinah
Al-Jami’-us-Sagheer, Dar- ul -Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Al-Kamil fi Du’afa-ir-Rijaal, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Al-Mu’jam-ul-Kabeer, Dar Ihya-ut-Turas Al-‘Arabi, Beirut
Anwaar Jamal-e-Mustafa, Shabbir Brothers, Lahore
Attargheeb Wattarheeb, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Bahar-e-Shari’at, Maktaba-tul-Madinah, Karachi
Fatawa Razawiyyah, Raza Foundation, Lahore
Haashiyah Tahtaawi, Karachi
Hayat-ul-Haywan, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Ibn Bishkwal, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Ihya-ul-‘Uloom, Dar Saadir, Beirut
Jam’-ul-Jawami’, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Lawaqi-ul-Anwaar, Dar Ihya-ut-Turas Al-‘Arabi, Beirut
Malfuzaat A’la Hadrat, Maktaba-tul-Madinah, Karachi
Mirat-ul-Manajih, Ziya-ul-Quran Publications, Lahore
Musannaf Ibn Abi Shaybah, Dar-ul-Fikr, Beirut
Musnad Imam Ahmad Bin Hanbal, Dar-ul-Fikr, Beirut
Qoot-ul-Quloob, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Rad-dul-Muhtar, Dar-ul-Ma’rifah, Beirut
Sahih Bukhari, Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah, Beirut
Sahih Muslim, Dar Ibn Hazm, Beirut
Sharh-ul-Muhazzab, Dar-ul-Fikr, Beirut



www.dawateislami.net

Shu'ab-ul-Iman, Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah, Beirut
Sunan-ut-Tirmizi, Dar-ul-Fikr, Beirut

Mwangaza Mkuu wa Kiroho na Kielimu wa karne ya 21,Allamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qaadiri Razavi دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه ameanzisha Dawat- e -Islami (vuguvugu la kimataifa lisilo la kisiasa kwa ajili ya kuhubiri Qur'an na Sunnah) linaloeneza mafundisho ya kiislamu katika nyanja zaidi ya 100 za maisha. Ukitaka kujua kuhusu Mwanzilishi wa Dawat- e -Islami, vitabu vyake, vijitabu, na idara mbalimbali za Dawat-e-Islami, basi tembelea tovuti hii: www.dawateislami.net.

Zaidi ya hayo, Dawat- e -Islami pia inaeneza ujumbe wa Uislamu duniani kote na Idhaa ya Madani, chaneli ya Kiislamu 100%. Haijalishi popote ulipo duniani, ikiwa ungependa kutazama Madani Channel, basi fuata masafa uliyopewa. Ikiwa unataka kuwasiliana nasi, basi tutumie barua pepe: overseas@dawateislami.net

## Idhaa ya Madani - Vigezo vya Ufunikaji Ulimwenguni

**Usambazaji:** Dijitali

| Satellite | Aina ya Boriti | Nafasi | Kiungo cha chini | Hz. | Polarity | Sym. Kiwango | FEC |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Asiasat (A7-C3V) | Global | 105.5 E | C-Band | 3739 | Vertical | 2815 | 3/4 |
| Intelsat 20 | Africa Region | 68.5 E | KU-Band | 12562 | Horizontal | 26657 | 2/3 |
| Eutelsat 7 | Middle East | 7 West A | KU-Band | 10815 | Horizontal | 27500 | 5/6 |
| Astra 2F | Europe | 28.5 E | Sky Platform | 12640 | Vertical | 22000 | 5/6 |
| Galaxy 19 | USA | 97 West | KU-Band | 121835 | Horizontal | 22000 | 3/4 |

اَلْحَمْدُ لِلّٰہِ رَبِّ الْعٰلَمِیْنَ وَالصَّلٰوۃُ وَالسَّلَامُ عَلٰی سَیِّدِ الْمُرْسَلِیْنَ اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰہِ مِنَ الشَّیْطٰنِ الرَّجِیْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰہِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ ؕ

# It is Sunnah for a traveller to keep 8 things with him

The blessed father of the Imam of the Ahl-us-Sunnah, Imam Ahmad Raza Khan, Maulana Naqi 'Ali Khan رَحْمَۃُ اللّٰہِ تَعَالٰی عَلَیْہ has stated: The Beloved Rasool صَلَّی اللّٰہُ تَعَالٰی عَلَیْہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم used to keep 8 things with him whilst travelling: (1) Miswak (2) Kohl (3) Mirror (4) Comb (5) Scissors (6) Needle (7) Thread. (Anwaar Jamal-e-Mustafa, pp. 160). In another narration, (8) 'Oil' is (also) mentioned. (Subul-ul-Huda, vol. 7, pp. 347)

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213
Web: www.maktabatulmadinah.com | E-mail: feedback@maktabatulmadinah.com